Ukombozi Mkamilifu

Sikujua la kusema asubuhi hii. Nilikuwa nimeketi nyuma huko pamoja na Ndugu Egan nami nilisikia...Ndugu Neville alikuwa akisema jambo fulani na kunitazama, nami nilimuuliza Ndugu Egan, "Je, ananiita?" Naye akasema, "Ndivyo."

2 Ndiposa niko hapa juu kunena jambo fulani asubuhi hii. Nilikuwa nikiwaza nilipokuwa...Ile pepeo pale ambapo inapunguza sauti, inaonekana inaipunguza kabisa unaponena na yaonekana kuwa ile pepeo inaitwaa sauti moja kwa moja. Nilikuwa nikisikia ushuhuda nilipokuwa ndani humo nikimwombea huyu mwanamke kwa simu, na yule aliyepokea ujumbe alisahau kuacha jina la mji ambao simu ingepigwa, toka kwa mke wa Daktari Morrison. Nami nitasema tu kile nimewatendea ninyi—yote ni maombi, na yangu, niliwekelea simu mikono kuelekeza nambari popote ilipokua, na nikamwomba Roho mtakatifu kumwendea yule mwanamke. Kwa hivyo nadhani yeye atasikia hayo jinsi angalisikia kama tungali...Maona? Nami niliiweka chini. Huenda ikawa hivyo ndivyo Bwana alivyotaka. Waona? Labda ingukuwa bora hivyo.

3 Ndiposa nilisikia shuhuda wakati nilipokuwa ndani humo. Mtu fulani akisema kuwa Dada Rook alikuwa na...naamini Ndugu Neville alisema kuwa yeye alikuwa amepatwa na kitu kama kuzimia kwa akili, kitu kama hicho. Na tumtumainie Mungu kwa hilo, tukikumbuka tu jambo hili moja, Mungu awajua walio wake. Yeye anajua habari zao zote.

4 Je, mnasikia vizuri huko nyuma? Ikiwa hamwezi, kuna viti vitupu hapa, mwaweza kubadilisha mkipenda. Na hebu tuone, je, hii ndiyo maikrofoni kuu? Hii hapa ndiyo maikrofoni kuu? Vema. Tutaona ikiwa tutaweza kuirudisha hiyo karibu kidogo. Na papa hapa je, Gene? Hivyo itakuwa vyema tu. Na mara nyingine mimi hupwewa na sauti. Nimekuwa nikihubiri kwa muda sana...Hiyo ni bora sasa? Mwaweza kunisikia vema?

5 Nasi bila shaka twakumbuka haya katika maombi. Na tunataka kutoa taarifa ya mkutano mzuri sana chini huko... Je, nimamtazama Dada Rook? Nilidhani nilimwona mwanamke nyuma huko aliyefanana naye. Nilidhani, "Hakika sizungumzi kuwili hapa." Ninamtazama mtu fulani anayefanana naye, kutoka upande wa nyuma. Yeye yuko katika Hospitali ya Mtakatifu Edward.

6 Na kwa hivyo huko Cleveland, Tennessee, na pia katika California, tulikuwa na mikutano mizuri. Bwana aliibariki sana, kwa mambo mengi yeye aliyoyatenda. Nasi twafurahi kwa ajili ya hayo. Nasi tuna furaha twaweza kurudi kwenye kundi

letu, tukitangaza wema wa rehema za Mungu. Hivyo ndivyo walivyofanya katika Biblia.

7 Nilikuwa nikimfurahia Ndugu Neville. . .au maombi ya Ndugu Beeler, jinsi yeye alivyowaombea watu, na—na akiomba msaada na rehema. Na tukitazama tu kote, ninyi kila mara, kila kitu kinachoendelea, mtatambua kuwa kuna kitu fulani halisi sana kwake. Na wakati ule Ndugu Neville alipokuja na kuwaleta mbele mashemasi na kadhalika hapa jukwaani, ku—kuomba baraka za Mungu juu ya—ya sadaka ya kanisa, nilimsikia akiomba Mungu dua kuhusu watu hao, jinsi walivyoombeana mmoja kwa mwingine. Na hilo lanifurahisha kusikia mchungaji anayewaombea mashemasi wake, na mashemasi wakimwombea mchungaji. Uonapo kanisa likishirikiana hivyo, naaam, kitu fulani ki tayari kutendeka. Hivyo ndivyo ipasavyo kanisa liwe kwa utaratibu. Na lilinipa tu wazo la fungu la fundisho. Nilitaka kunena juu ya zile baraka kule Kadeshi, na kule kukataa, kusikia taarifa ya wale wapelelezi, lakini nikabadili nia yangu kuzungumzia jambo lingine basi.

8 Na sasa, kuhusu uponyaji, nina ushuhuda mdogo ambago ningependa kutoa. Nilitumaini ningemwona mwanangu, Billy, nyuma huko, lakini yeye anayo mfukoni mwake. Na Billy ameanza kuwa bora mikutanoni zaidi ya vile alivyowahi kuwa. Yeye alikuwa mwenye wasiwasi na fadhaa, na angewaambia watu, "Jamani, nendeni mketi, nendeni mketi chini." Kasema, "Nita—nitawapa kadi za maombi." Lakini nimeona hivi majuzi kumeanza kuwa na watu mkutanoni anaowasikitikia, iwapo hajabakiza kadi za wanaohitaji maombi, basi angewaweka chumbani ili niende kuwaombea.

9 Na jambo kama hilo lilitendeka huko Chicago wakati wa mwisho, nami ningependa kusoma barua hiyo yeye akiingia. Sikuwahi kumwona. Yeye hakujua nilikuwa nikija asubuhi hii, huku, na nataka—nataka barua hiyo. Lakini nilifikiri tu juu yake nilipowaza juu ya wingi wa magonjwa. Na hivi ndivyo ilivyo. Ni barua iliyothibitishwa niliyokuwa nikiisoma gazetini (Sikuisoma; niliambiwa), ya kwamba magazeti yalikuwa yakimshutumu Oral Roberts kwa kumwombea mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa sukari na akafa. Nami, si nje ya . . . kama Mwamerika, ninapenda kutii sheria na—na mtu aliyeko mamlakani, lakini nafikiri hiyo si haki. Nashangaa ikiwa wangependa kuandika gazetini wote ambao Oral Roberts amewaombea na wakapona, ambao madaktari walikuwa wamewakatia tamaa. Nashangaa ikiwa wangebadilisha tu mara moja, mwaona. Hawangeweza kufanya hivyo. Ndiposa nadhani labda Shetani amewafarakanisha hivyo hata, Mungu akipenda, katika Siku ya Hukumu, itawabidi wajibu kwa ajili ya hayo. Lakini najua maelfu ya watu ambao Oral Roberts amewaombea, ambao wangalikufa nao ni wazima.

10 Kwa hivyo mnaona, wao hawatendi haki juu ya hilo. Wao watatoa upande wao, wa lawama, bali hawatatoa upande ule mwingine. Sasa, gazeti lapaswa kuwajulisha wananchi mambo yanayotukia. Basi nafikiri ikiwa wanadamu wanahusika mmoja kwa mwingine, mtu fulani akiponywa, kuponywa kabisa, kila gazeti katika Amerika lapaswa kuandika habari zake. Lakini huwezi kuwaajirisha walifanye hivyo. La, ukipeleka kitu kama hicho huko, wao watachekelea kipumbavu na kudharau na kukataa, lakini sasa ikiwa kuna kitu cho chote cha kulaumu. Yaonyesha tu kuwa taifa hili li tayari kuhukumiwa. Naam. Na patakuwa na hukumu, na hakuna njia ya kuiepa, nao wanajiwekea tu moto juu ya vichwa vyao, na kadhalika, ni—ni mafarakano ya kanuni jinsi gani. Gazeti, kanuni zake ni ku—kupasha habari wananchi huhusu cho chote kizuri au kibaya kinachotendeka. Lakini wao wako mbali na kanuni zao. Na wakiwa mbali na kanuni zao, basi wao—wao hawatatumikia kusudi lao vema.

11 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa. Kanisa liwapo mbali na kununi zake, haliwezi kamwe kutumikia watakatifu vyema. Yatupasa tuwe pamoja, yatupasa tuungane. Yatupasa tuwe na moyo mmoja na nia moja. La sivyo, hatutamtumikia Mungu kamwe au watu tusipokuwa na moyo mmoja na nia moja, kusimama kwa kanuni za Biblia na mambo ambayo Mungu amesema ambayo ni kweli. Yatupasa kila mara kuyazingatia.

12 Billy alikawia chumbani huko Chicago, yeye . . . Mtu fulani akamjia, mwanamke na mumewe, akiwa na kansa mapafuni, akifa, na mke wake alikuwa anaugua kupooza amelazwa kwenye kiti chenye magurudumu, naye akijaribu kumtunza mume huyo ambaye ilikuwa vigumu kwake kusimama, akiwa na kansa mapafuni mwake. Na Billy akamwambia, akisema, "Na—nasikitika, bwana." Kasema, "Ningekupa kwa furaha kadi ya maombi." Pia akasema, "Lakini si—sina nyingine iliyobaki."

13 Yule mtu kasema, "Vema, haidhuru, mwanangu." Yeye kasema, "Hilo ni njema." Kasema, "Tumejaribu kufika hapa, lakini ilikuwa vigumu sana kwetu."

14 Billy kasema, "Nitakwambia la kufanya." Kasema, "Ninaenda kumwita baba na nitamleta ndani, nami nitamtoa nje." Na kasema, "Nifanyapo hivyo, mara tu msikiapo ujumbe wake," kasema, "ndipo mlete mkeo . . . au uje pamoja na mke wako, na uingie katika chumba kidogo pale nilipopitia, nami nitamwambia awaombee."

15 "Lo!" yeye alisema, "huo ni uaminifu, mwanangu. Hilo ni zuri vya kutosha. Mwaona?" M—msimamo ndio huo, mwaona. "Nzuri vya kutosha. Hivyo ni vema." Mwaona?

16 Na usiku huo, Billy, aliporudi huko, bado akiwa kinyume cha kile alikuwa amesema, kuwa yuna shemeji yake hapo aliyekuwa akitokwa na damu akiwa na ugonjwa wa mtoko wa damu

mapafuni, na shemeji yake wa kike aliyekuwa akitokwa na damu tumboni akiwa na vidonda, pia kwamba wao walikuwa wameingia pamoja nao, ili kuwasaidia waingie. Yakupasa uwe mwangalifu, wangejaza chumba chote, mwaona. Lakini tulipokuja na kuwaombea, tulipata habari kwa barua kuwa huyo mtu amepona kabisa kansa ya mapafu; yule mwanamke, yule mkewe katika kiti chenye magurudumu amesimama akitembea kawaida kabisa; yule mtu aliyekuwa na mtoko wa damu kwenye—kwenye mapafu kutokana na kifua kikuu amepona kabisa, na mke wake amepona vidonda vya tumbo. Wote wanne waliponywa mara moja; nashangaa ikiwa magazeti yangekubali kuchapisha hayo. Mwaona? Mwaona? Jamani, lakini Mungu yuangali ni Mungu. Yeye hutenda tu mambo katika njia yake mwenyewe, mwajua, naye yu mwema sana. Tuna furaha tele kujua kuwa yeye ni Mungu.

17 Tulikuwa tukinena asubuhi iliyopita kuhusu mhubiri mdogo tumjuaye aliyekuwa akishuka kwenda kuwaombea wagonjwa na kadhalika, naye alienda na kumwombea mtu fulani hospitalini huko Louisville, akiwa na ugonjwa wa kifua kikuu, huyo mwanamke akafa. Maskini mtu huyo akasema, "Vema, hakuna haja...Mungu hayuko...Hakuna Mungu, yeye angetimiza Neno Lake." Kasema, "Nilimpaka tu mafuta kama—kama Biblia ilivyosema. Yeye asipolitimiza Neno lake, yeye si Mungu." Kasema, "Ni kitabu tu."

18 Sasa, hilo lingeonekana hivyo isipokuwa uwe unamjua Mungu. Hiyo ni sehemu ya Maandiko, bali sio Maandiko yote. Ni juu ya msingi wa imani ya mtu binafsi. Unaona?

19 Nimi nilimwambia mke wangu, na kusema "Kumekuwa na mambo mengi yaliyotendeka, ambayo kwayo najua kuwa yuko. Sijui kipi kitakachotendeka kwangu mwishoni. Huenda nikaiendea njia ile ile. Kama Mungu akiondoa mkono wake wa rehema kwangu, nitaiendea njia ile ile. Lakini mradi Yeye ameuweka mkono wake wa rehema na uongozi juu yangu, nitaendelea." Lakini nilimwuliza Meda, nikamwambia, "Ni nani yule aliyekuwa chumbani hiyo asubuhi baada ya lile ono langu nilipomwona binti yangu mdogo, Sharon?"

20 Licha ya hayo, hivi majuzi, ningalizirai, nilikuwa nimeketi kwenye barabara ya mji. Nanyi mwajua hadithi yangu baada ya ono lake...Nilitazama akija kando yangu, na hapo kukaja msichana mdogo kwenye njia ya mji hapa Jeffersonville, ilikuwa tu kama lile ono. Ilinilazimu tu kushikamanisha mikono yangu pamoja. Ilionekana kabisa kama ono lile la mtoto wangu Sharon; yeye alikuwa mwanamke kijana wakati huo.

21 Na baada ya ono lile asubuhi hiyo nilipokuwa Utukufuni, ni...Hope alikuwa akiniambia, na huku amenishika begani akisema, "Usitufadhaikie, Bill. Tu heri sana." Nilikuwa tu

najaribu kujiuwa. Naye akasema, “Usifadhaike. Niahidi hutafadhaika tena.”

22 Nami nilisema, “Siwezi kuahidi hilo, Hope, kwa sababu ni—ni—nina—ninafadhaika. Siwezi kujizuia.”

23 Nami nilitoka kwenye ono hilo, nikisimama katika chumba chenye giza. Na sio ono, sio kuwazia, lakini alikuwa angali amenishika begani. Na yeye alikuwa akinipapasa. Nilidhani, “Ngoja kidogo. Hili sio . . .” Sikujua la kuliita siku zile, ono, nililiita njozi. Nilisema, “Huu ni mkono wake ukiwa ungali hapo.” Nilisema, “Je, uko hapa Hope?”

24 Yeye akasema, “Bill, niahidi kuwa hutafadhaika tena kunihusu mimi na Sharon.” Sababu nilikuwa nimekata tamaa, nilikuwa tayari kujiva. Nilisema, “Nakuahidi.” Na yeye akanikumbatia na kunipapasa kwa mkono wake. Ndiposa ni—nilisema, “Hope, uko wapi?” Nilipata . . . nilipapasa-papasa na nikashika ile nyororo ndogo ya taa na kuivuta. Nikazunguka-zunguka, nikamtafuta katika kila kiti kuona kama yeye ameketi hapo. Yeye ni Mungu. Yeye ni Mungu leo kama tu alivyokuwa Mungu kwenye huo Mlima wa kugeuzwa Kwake Yesu faraghani Musa na Eliya walipotokea. Yeye yuangali Mungu.

25 Huenda tukapitia katika masumbuko na majaribu mengi. Kumbukeni tu, kunaye Mtu fulani ajuaye, huangaza njia, huifanya halisi. Sijui yaliyo nyuma ya pazia, ila najua jambo moja, nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu, kila siku nikijaribu kuishia lile jambo kuu litakalotendeka siku moja nitakapomwona yeye uso kwa uso na nisimulie hadithi ya kuokolewa kwa neema. Hiyo ndiyo siku ninayoiishia. Nikiyasahau yaliyo nyuma, mambo yaliyoko, nataka kukaza mwendo, nikiendelea tu.

26 Nataka maskani haya, kwani sasa mumesimama, nataka mkaze mwendo muifikilie ile mede ya thawabu ya mwito mkuu. Cho chote mtendacho, shikamaneni, iweni na undugu mwezavyo kuwa, lakini kila siku mkiwa na mkono ulionyoshwa mfikieni na kumpata mtu mwingine mumwingize ndani. Lakini katika Imani hii tunayoihubiri sasa na kuishindania kwa juhudi, msisonge mbali nayo hata inchi moja. Maana, kama mnaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, huu ni mpango wa Mungu! Hautakuwa katika wingi. Kila wakati utakuwa katika uchache, imekuwa vivyo hivyo kila wakati na utakuwa hivyo daima, Lakini kumbukeni, imeandikwa, “Msiogope, enyi kundi ndogo, kwa kuwa Baba yenu ameona vema kuwapa ule Ufalme.”

27 Sasa, kuna afisi nyingi za kanisa letu, mashemasi, wadhamini, msimamizi wa shule ya Jumapili, mchungaji, katika utaratibu wa kanisa. Nanyi ndio mliowachagua maafisa hawa pamoja na mchungaji huyu. Mimi ni msimamizi wa yote, kuona kwamba inaandelea vyema, na kuwashauri na kadhalika. Ninyi ndio mnaomchagua mchungaji wenu, mnawachagua

wadhamini wenu, mnawachagua mashemasi wenu, mwachagua kila huduma iliyoko katika kanisa hili, ninyi watu. Na ni wajibu wenu kuwasaidia watu hao, mwaona, maana watafanya makosa. Wao ni wanadamu, wao ni watu tu, nao watafanya makosa. Lakini Rais wa Amerika akifanya kosa, je, twamtupilia bali kama Rais? Tunalisahau na kuendelea. Hivyo ndivyo tunavyotaka kufanyia kanisa letu sasa. Nilikuwa nikimsikiza yeye dakika chache zilizopita akiombea mashamasi, na nikasikia ushuhuda mle nyuma, mlangoni, toka kwa wadhamini, jinsi nyote mlivyo na nia moja. Sasa mwe tu hivyo. Sasa, ninyi washiriki wasaidieni hawa wadhamini na mashemasi na mchungaji. Na kumbukeni, mkiwa pamoja hivi, kumbukeni kuwa kazi ya Shetani ni kuona kuwa huo umoja umevunjwa. Naam, imekuwa vile kila mara na itakuwa hivyo daima. Lakini ninyi waungeni mkono wahudumu wenu, na hayo ndiyo niliyotaka kusema.

28 Ndiposa hapa tena ninacho pia—kitu fulani cha kuwekwa kwenye ubao wa matangazo asubuhi hii, kuhusu mkutano wa halmashauri na wenye mamlaka. Na itakuwa kwenye ubao wa matangazo nami niliipata nakili ya Ndugu Roberson aliye mwenye kiti wa—wa wadhamini. Na pia nina nakili ya Ndugu Collins, nadhani, anayeshikilia mahali pa mwenye kiti wa halmashauri ya mashemasi. Na sasa, afisi hizi zote zimewekwa kulingana na Maandiko, na lazima wawe na kanuni za Kimaandiko kuhusu yale wapaswayo kutenda. Kwa hivyo, wadhamini wana huduma yao wenyewe. Na mashemasi wana huduma yao wenywewe. Msimamizi wa shule ya Jumapili ana huduma yake. Naye mchungaji ndiye mkuu wa kundi.

29 Sasa, kila moja ya hizi inashirikiana. Nami nafikiri kuwa mikutano yenu haipaswi kuwa pamoja, lakini yapaswa iwe mbali mbali, kwa maana, mashemasi hawana cho chote cha kuwaambia wadhamini isipokuwa wao wawe na habari za kuwapasha wao. Hali kadhalika, wadhamini wanahusika na hazina na mambo ya ujenzi, hawana cho chote kinachowahusu mashemasi. Mashemasi ni askari wa kanisa na wasaidizi wa mchungaji. Nao wadhamini ndio walindao mali yote. Wadhamini hawashughulikii mambo ya kiroho kamwe, shemasi hashughulikii mambo ya fedha. Kwa hivyo, lazima iwe hivyo. Na msimamizi wa shule ya Jumapili anasimamia shule ya Jumapili. Kwa hivyo nimeandika yote, imepigwa chapa, ili iwe kwenye ubao wa matangazo.

30 Ndiposa tutakuwa na muhtasari wa mafundisho yanayoshikiliwa na kanisa hili, tuyaweke kwenye fremu hapa kanisani; kile tunachoshikilia, ka—kanuni, mafundisho ya kanisa. Naam, ili tuwe kanisa, lazima tuwe na mafundisho.

31 Hatupigilii kigingi na kusema tu, "Tutaendelea mpaka umbali huu." Tutaendelea tu kushiriki pamoja na kila mmoja ambaye Mungu atatuwezesha kuingia pamoja naye Maandikoni

Mwake. Na sasa mwe pamoja, mwe na nia moja, moyo mmoja, mkamtumikie Mungu. Hivyo ndiyo Mungu anavyotaka tutende. Sasa na tuombe ndiposa tufungue Neno.

32 Ee Bwana mpendwa, sisi tuko karibu sasa kuliendea Neno la Kiungu au kulisoma Neno hili. Na Roho wako Mtakatifu atufafanulie sisi yale tunayohitaji. Na turuhusu tunene, Bwana, na kutenda na kuishi, tukijua kuwa sisi sote tu watoto Wako, kwa neema, kama ulivyotuita sisi. Na kuwe na ushirika kanisani humu, kwa kuwa tuko tayari tu kuingia katika mwenendo mkuu, twajisikia, kama kuwaleta wahudumu wengine waende kule nje ambako, kama utanituma huko, sehemu mbalimbali duniani, kuimarisha Imani, na kuwa na mhudumu aliye tayari na anayetaka, na aliyetayarishwa kusimamia. Na ile imani waliyokabidhiwa watakatifu, ambayo twaishikilia kwa ushujaa, iwe duara kuizunguka dunia. Tujalie, Bwana. Na fungu hili ndogo la kwekwe kama palivyokuwa siku moja tulipopaweka wakfu Kwako, na pawe na kanisa hapa, Bwana, ili toka kwalo watoke wahudumu na wainjilisti na waalimu na wamishenari watakaoenda sehemu zote za ulimwengu.

33 Tungeomba asubuhi hii, baraka maalum kwa Ndugu wetu na Dada Stricker wanaougua sasa. Lakini twajua kuwa sisi sote tumewekwa kwa majaribu haya. Kila mwana amjiaye Mungu lazima arudiwe, ajaribiwe. Na tukikata tamaa upesi, na kurudi nyuma, basi sisi tu wana haramu, na si wana wa Mungu. Wape Ndugu na Dada Stricker nguvu, na uwezo, wazidi kutimiza wajibu wao. Ikiwa wataomba chakula walacho, na mkono Wako wa baraka uwe juu yao. Maana hatujui huenda ikawa ni kwa juhudi iyo hiyo utawaonyesha hao wenyeji wa Afrika jinsi Mkristo halisi alivyo. Liruhusu, Bwana. Sasa na yote yatendeke kwa mapenzi yako.

34 Mbariki mchungaji huyu, Ndugu Neville. Twaomba, Bwana, kuwa utamfanya mchungaji wa hili kundi, kama ulivyofanya wakati uliopita. Nasi hatungesahau mke wake mpendwa aliye mgonjwa sana. Adui angependa kumwacha Ndugu Neville na kundi hilo la watoto, pasipo mama, lakini twasimama na kuweka, kwa imani, Damu ya Yesu Kristo kati ya adui na dada wetu. Na Roho Wako, Bwana, awe kwa wingi juu yake, tukijua kuwa wanawake wote wamewekwa kuishi chini hapa katika bonde hili, la giza la wakati huu, lakini twaomba kuwa utakuwa pamoja naye. Wabariki hao watoto wadogo. Yeye atakuwa na wasiwasi sasa na kuhuzunika, lakini Roho Mtakatifu na awe mlangoni mwa rehema wakati wote kwa ajili ya jamaa hiyo.

35 Bariki halmashauri yetu ya wadhamini, Ndugu Wood pale na Ndugu wetu Egan, Ndugu Roberson, na wengine wote, Bwana. Mashemasi, wadhamini, nao wote wanaohusika kanisani, twaomba, Bwana, kuwa utawaruhusu wao watumikie muda wao kwa utakatifu na—na haki. Wabariki wale, Bwana, waliotumika kwa wakati uliopita. Nasi twaomba kuwa utaendelea kuwa

pamoja nasi sote ili tujulikane kama kanisa la umoja na roho na upendo wa Bwana. Twaomba sasa kuwa utatumegea Neno kama tunavyohitaji, tunaposoma toka kwa Neno lako lililoandikwa. Maana twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

36 Katika kuomba, nilikuwa nikiwaza wakati tunapobariki au kuomba baraka kwa ajili ya hii yetu ya kisasa. . . halmashauri yetu mpya ya wadhamini na kadhalika, nilikuwa nikiwaza kuhusu Ndugu Fleeman na Ndugu Deakman na wengineo wanaoketi hapa, ambao wametumika vema mbeleni. Nasi twataka kumshukuru Mungu kwa ajili ya utumishi wao bora. Na Mungu awe pamoja nao daima na awabariki na kuwasaidia. Nataka kusoma kabla. . . Hebu kumbukeni tu sasa, matangazo yaliyo ubaoni na kadhalika, na mkutano ujao.

37 Nasi tuna furaha kuwa pamoja nasi asubuhi hii, vema huenda nikaisema hivi, mtu ambaye kwangu amekuwa wa dhamani sana kwa wakati uliopita, na angali wa dhamani sasa, ndugu mwema, Fred Sothmann kutoka. . . na mke wake, kutoka Sasketchewan, Canada, aliye hapa kututembelea sisi. Nchini mwetu, mgeni; lakini katika ushirika wetu, ndugu mpendwa, Ndugu Fred Sothman anayeketi pale. Yeye husimamia mikutano yangu niwako huko Canada.

38 Na ndugu mwingine mpendwa ambaye hapo awali alikuwa mwenyeji wa Canada, alikuwa mfanyi biashara, naye aweza kuuthibitishia ulimwengu kuwa huwezi kutoa zaidi ya Mungu. Yeye na mwenziwe waliunda wakfu wa fedha za ujenzi, au wakfu wa kazi katika nchi za ng'ambo; wakfu. Nao waliniita huko Oakland kwa ajili ya mkutano, na kusema wao walikuwa na pesa, nao wangeugharimia wote kwa wakfu wao.

39 Mimi na Ndugu Fred tulijaribu hayo kwa pesa fulani ambazo Ndugu Fred alikuwa nazo ambazo singeweza kuzichukua kama mtu binafsi. Kwa hivyo basi tuliamua tungezitoa kwa watu wa Canada na hata tusichukue sadaka, lakini haikuendelea vema. Mikutano ilikuwa mizuri, lakini kwa sababu hatukuchukua sadaka. . . Sijali hata ikiwa kanisa ni la dhamani ya dolla bilioni mia, bado utahitajika na Mungu kuchukua sadaka. Hiyo ni sehemu ya ibada. Nanyi mwamwibia hiyo. . . Hata kwa kadiri nilivyochukia pesa na mambo kama hayo, natambua mtu akoseapo heri ukubali kuwa umekosea, kwa sababu mimi na Ndugu Fred tumeona kwamba matokeo yake si mazuri.

40 Na, Ndugu Borders nilipomwacha Ndugu Fred nikaja kwako wewe huko Oakland, nilisema, "Usifanye hayo, wewe pitisha tu kisahani cha matoleo na uchukue sadaka, na, hata iwe ni kiasi gani, iweke kwa wakfu wenu kwa mkutano mwingine mahali fulani."

41 Na kabla mikutano haijakwisha Ndugu Borders na rafiki yake walinijia na kusema, "Kiasi tulichotumia katika mkutano, kimekusanywa."

42 Ndiposa siku chache zilizopita yeye alifanya mpango wa mkutano huko San Jose, California, ambapo alikuwa na baadhi ya, nadhani makanisa sitini au sabini huko bondeni, ya imani zote mbalimbali yakishirikiana. Tulikuwa na mkutano wa ajabu, na tunarudi tena Novemba. Tuna furaha kuwa pamoja nanyi Ndugu Borders na Ndugu Fred anayeketi nyuma huko. Na watu hawa wana. . .labda ni wageni kwenu nyote lakini wamekuwa ndugu wapendwa kwangu nje huko, wakishindania kwa bidii ile Imani tunayoishikilia. Mungu awabariki, ndugu zanguni. Tuna furaha kuwa nanyi asubuhi hii katika maskani haya madogo na yaliyochakaa, si ya kuvutia, lakini kuna kitu fulani tujuacho hapa, nacho ni kwamba Mungu aishi hapa, mwaona. Kwa hivyo tuna furaha kwa ajili ya hilo. Na kuna ndugu wengine wapendwa sana, kama ningalikuwa na wakati ningewataja, walioko pamoja nasi leo.

43 Sasa ninatarajia sana na kuomba kuwa katika siku chache zijazo, Bwana akipenda, nataka kwenda, nasikia nikiongozwa, sijatangaza bado mkutano utakaofuata, hadi Ohio, kuwa na Ndugu Sullivan huko kambini, baada ya muda mchache. Ni karibu maili mia juu hapo, nakisia, Gene, kitu kama hicho. Itakuwa safari nzuri ikiwa ulikuwa hujapanga mapunziko yako. Bwana akizidi kutuongoza. Mtu mwema sana, nasi twapendezwa na Ndugu Sullivan sana sana. Yeye, yeye ni meya wa mji huo, naye alikuwa meya na ni mtu wa mtindo wa kikale wa Kentucky. Hayo tu ndiyo ninayoweza kusema kumhusu. Nilipomkuta siku moja katika. . .Sote tulilelewa huko milimani ya Kentucky, yeye aliniambia, "Je, ungali una mvuje wako shingoni, Billy?" Sasa mwajua jinsi alivyo Mkentucky. Sasa tufungue katika. . .Siwadharau ndugu zangu hapa wa Kentucky, Ndugu Jeffreys na wengineo. Mimi pia ni Mkentucky, ninyi mwajua. Nawaambieni tu kitu kimoja ambacho tuko, sisi si wa—Kentucky wala Waamerika; sisi ni wasafiri na wageni; twatafuta mji ujao.

44 Kwa somo, hebu na tusome kitabu cha Kutoka kwa dakika chache. Natarajia kusoma sura ya 23, na kifungu cha 20 hadi cha 23, chote pia. Nami nataka kuchukua somo asubuhi hii hivi kama hili, samahani, Ukumbozi Mkamilifu. Nami sitahubiri kwa muda mrefu sana sasa hali nikiwangoja mfungue kitabu chenu na sura yake.

> *Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokutengenezea.*
>
> *Jitunzeni mbele yake,. . .mwisikize sauti yake; wala msimtie kisirani; maana, hatawasamehe makosa yenu; kwa kuwa jina langu limo ndani yake.* (Nina hakika kuwa kusanyiko hili linajua huyu malaika alikuwa nani). . .*jina langu limo ndani yake.*

Lakini ukiisikia sauti yake kweli, na kuyatenda yote ninenayo mimi; ndipo mimi nitakuwa ni adui wa adui zako, na mtesi wa hao wakutesao.

Kwa kuwa malaika wangu atatangulia mbele yako, na kukufikisha. . .kwenye Mwamori. . .na Mhiti,. . . na Mperizi, na Mkanaani,. . .na Mhivi, na. . .Myebusi; nami nitawakatilia mbali.

45 Na Bwana abariki Neno lake tunaponena sasa kwa dakika chache, ikiwa mngeomba. Nilikuwa nikiwaza kuhusu somo hili la *Ukombozi Mkamilifu*. Kanisa limekuwa katika—katika uchache. Litakuwa vile kila mara, katika washiriki, hadi Yesu ajapo. Lakini linaishi chini ya heshima zake lililopewa na Mungu. Laiti tungalijua tu, kuwa hili ni kanisa la Mungu aishiye, si Maskani ya Branham, maana Maskani ya Branham ni shemu yake tu. Kunayo maskani mengine kama haya kote nchini.

46 Ndugu Snelling usiku huu atakuwa na ibada ya ubatizo, nilisahau Ndugu Curtis aliniambia nitangaze hilo, ama aliniambia jana yeye atakuwa nayo. Yeye atakuwa na ibada ya ubatizo, na ikiwa kuna ye yote hapa ambaye hajawahi kubatizwa bado, naam, Ndugu Snelling atafurahi kufanya hivyo usiku wa leo. Hayo ni Maskani ya Utakatifu huko Utica. Na Ndugu Junior Jackson huku New Albany. Na kunayo makanisa kama haya kote nchini, lakini sote tunaishi, yaonekana, upande ulioshindwa, kwa kadiri.

47 Nilisikia Ndugu Neville akitangaza asubuhi hii nyuma huko, ikaja bongoni mwangu, kuwa yaonekana watu wanaenda mbali na ukombozi. Yaonekana kuwa kama kitu ambacho watu wamekiona kwa hivyo wao wanakisukumia upande mmoja, "Lo! vema, Mungu aweza kukifanya." Lakini hiyo siyo nia!

48 Sasa, Musa, alipoitwa na Mungu, yeye alikuwa hasa nabii kamili. Mungu amtumapo mtu atende cho chote, Yeye humkabidhi kila kitu anachokihitaji. Mungu amwitapo mtu awe mhubiri, Yeye huweka kitu fulani ndani yake cha kuhubiria. Akimwita kuwa mwalimu, Yeye huweka kitu fulani ndani yake cha kufundishia. Anapomwita kuwa nabii, Yeye huweka kitu fulani ndani yake kuona maono na kuwa nabii. Mungu daima humfanya tayari kabisa mtu Wake. Na hivyo ndivyo tu Yeye alitenda alipomtuma Musa huko Misri. Alimwinua katika njia fulani, na kumfundisha kwa njia fulani, na alimuunda na kumtengeneza na kumfanya. Baada ya kumuahidi Ibrahimu, mamia ya miaka hapo kabla, kuwa huyo angewakomboa hao watu ndipo Yeye—Yeye hata alikusudia kumfanya Musa jinsi tu Musa alivyofanywa. Musa alikuwa nabii kabisa. Ndiposa akiwa nabii kabisa. . .

49 Ndipo basi kama wewe, ikiwa u Mkristo. Mungu hawafanyi watu Wakristo nusu, Mungu huwafanya Wakristo kamili. Mungu hawafanyi wahubiri nusu, lakini mhubiri aweza kuwa nusu.

Na Mungu huwafanya watoto Wake Wakristo, lakini wakati mwingine wao huwa Wakristo nusu. Lakini si kusudi la Mungu wawe hivyo. Ni njia zao wenyewe zinazochanganyikana na mpango wa Mungu kwa maisha yao, na hilo ndilo liwafanyalo jinsi walivyo. Mungu hawataki wawe Wakristo nusu au wahubiri nusu wakipatana upande huu na ule. Au, Yeye anawataka wawe ambapo vita vimewaka moto!

50 Sasa, Musa, Mungu alikuwa amemfanya nabii kamili kwa ukombozi mkamilifu. Na Musa alikuwa amejitolea kabisa mikononi mwa Mungu. Hiyo ndiyo ilimfanya yeye jinsi alivyokuwa. Alikuwa mkamilifu sana hivi kwamba Mungu angemsadiki.

51 Nashangaa asubuhi hii, kama Wakristo, kama tumejitolea sana kwa mapenzi yetu wenyewe, na kujitolea wenyewe kabisa kwa Mungu, hivi kwamba Mungu anaweza kutuaminishia mahali ambapo Yeye ametuweka. Nashangaa asubuhi hii, kwangu mwenyewe, ikiwa ningalijisalimisha mbele za Mungu hivi kwamba Mungu angenitumaini, amtumaini Ndugu Neville, aitumaini halmashauri yetu ya wadhamini, halmashauri yetu ya mashemasi, washiriki we—wetu wa kanisa letu. Sisi sote tuna mahali fulani na tuna wajibu fulani.

52 Mhudumu ana wajibu wa kusimama na kuhubiri utajiri Wake Kristo usiopimika, pasipo kupatana, ikiwa yeye ameitwa awe mhubiri. Yeye hangeacha hata jambo moja kwa ajili ya mtu fulani ikiwa yeye ameitwa kuwa mhubiri.

53 Na mshiriki wa kanisa, yeye ameitwa awe mshiriki wa kundi fulani hili, basi yeye hangepatana. Ikiwa kanisa laamini kuwa haitupasi kucheza karata, basi mshiriki yule hapaswi hata kugusa jozi ya karata. Hatuamini katika kunywa pombe, hana budi kugeuza kichwa chake kabisa kutoka kwa ulevi. Ikiwa hatuamini katika kucheza kamari wala kuvuta sigara, mshiriki wa kanisa hili hapaswi kugusa kitu kama hicho. Mungu hutoa ukombozi mkamilifu wakati sisi . . . Yeye atafanya hivyo ikiwa tutajitolea Kwake kabisa sisi wenyewe. Ikiwa tutajiweka kabisa mkononi Mwake, ndiposa Mungu anaweza kuishi ndani yetu, Kristo Tumaini la Utukufu. Yeye aweza kujioyesha mwenyewe toka kwetu tunapojiondoa wenyewe njiani ndipo mawazo yetu ni mawazo Yake. Je, ungewaza Kristo akivuta sigara? Je, ungewaza Kristo akinywa pombe wala akicheza karata? Basi ikiwa roho yako ni sehemu ya Roho Wake, Yeye ataka muungame hayo. Lakini ninyi humruhusu Shetani aingie na kutwaa mamlaka, na kila wakati mioyoni mwenu kabisa mwajua mnakosea mtendapo mambo hayo. Na mshiriki mmoja angenena juu ya mshiriki mwingine; mwajua hilo ni kosa. Mmeamriwa kuombeana mmoja kwa mwingine, si kunena dhidi ya mwingine, bali kupendana mmoja kwa mwingine. Na ikiwa mtu fulani ameanguka, na tumwinue, tumsaidie. Sasa, hilo latufanya sisi ku—ku—kundi lililounganika la waamini. Sasa, tusipotii hilo, basi hatumtiii

Mungu wala kumpendeza Mungu. Na kwa hivyo kanisa letu, watu wetu hawawezi kustawi, kanisa haliwezi kuendelea, ni kwa sababu hatujaunganika pamoja. Kama Yesu alivyosema, "Chachu kidogo hulichachua donge zima."

54 Sasa, ikiwa halmashauri ya kanisa, au kama ma—mashemasi wangekuja na kusema kuwa tunahitajika ku. . .wakiona inatupasa kujenga maskani mapya. Ikiwa hiyo ndiyo kura ya mashamasi, na wadhamini wamekwisha kupashwa habari nao hawana pesa za kujenga, halafu wao wana mpango wa ujenzi kama tulio nao ukiendelea sasa. Ndiposa inapelekwa kwa kusanyiko lote, kama itupasavyo kuwa, kanisa lote likiwa ndilo lenye mamlaka. Kwa hivyo ikiwa kanisa linapiga kura wakipendelea maskani mapya, ndipo sisi sote yatupasa kushirikiana pamoja katika kujenga hayo maskani mapya.

55 Kusema kweli, mimi mwenyewe, waliponena kuhusu maskani mapya kwangu, nilipinga wazo hilo. Naam. Nilisema, "Hatuhitaji hasa maskani mapya. Huenda nikaondoka hapa hivi karibuni kama Bwana. . .ikiwa yale aliyonionyesha yatatimia. Je, tunahitaji maskani mapya ya nini? Hatuna pesa."

56 Ndipo nilikuja na kuona maoni ya kanisa, ilionekana wingi wa kanisa ulipendelea jambo hilo. Basi nami nilifanyaje? Niliacha mafikara yangu na kuungana na kanisa. Hakika, hebu na tulijenge, ikiwa hivyo ndiyo tumepiga kura. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika wakati wa Biblia, jinsi kanisa lilivyopiga kura. Ma—mamlaka, yale makundi ya watu yalikusanyika pamoja. Katika umoja kuna nguvu. Kwa hivyo basi nilisema, "Hakika, kama hivyo ndivyo kanisa linataka, ikiwa ndivyo Mungu anataka, Yeye ana mamlaka zaidi ya kupiga kura katika kundi nzima la watu kuliko Yeye alivyo kwangu, kwa sababu sina ono la kusema kuwa isifanywe." Kwa hivyo tunakubaliana na kanisa, na kuendelea na kanisa. Nami ninashirikiana nalo kufanya lile niwezalo, waona, kusaidia kanisa.

57 Hiyo yapaswa kuwa nia ya kila Mkristo na kila mtu kanisani, ni kuungana pamoja na kuvumiliana. Cho chote kile kanisa lipigiacho kura, yatupasa kuambatana nacho. Basi tusema kwa mfano, wao wanataka kubadili kitu fulani kanisani. Vema, basi, iwapo wadhamini wanataka au mtu mwingine anataka kufanya hivyo, mashemasi, wanataka kubadili kitu fulani, hilo laletwa mbele ya kanisa, kanisa likiwa pamoja. Na ikiwa wazo le—letu hapa laonekana kuwa tofauti kidogo na kile kanisa lote liwazacho, na tutupilie mbali hilo wazo, kwa sababu hiyo tu ndiyo njia pekee tuwezayo kudumu katika huo umoja. Na ikiwa kanisa hili litaendelea tu mnavyoendelea sasa, na likiwa na umoja, Mungu ata. . .Atakayotenda hayana kikomo tukidumu pamoja. Yatubidi kuungana. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuwa, kuungana kikamilifu sisi kwa sisi, ndiposa tujitolee kikamilifu mikononi mwa Mungu.

58 Ndiposa yatupasa kuwa na mtu tunayeamini kuwa anahubiri Neno la Mungu. Mtu huyo asipofanya hilo, basi tafuteni mtu mwingine anayefanya hivyo. Hivyo ndivyo itupasavyo kukaa. Ikiwa halmashauri ya wadhamini haitashikilia yaliyo kweli, basi ni kazi yenu kuchagua mtu atakayeshikilia yaliyo kweli. Ndiposa, mfanyapo hivyo, lishikeni. Ni juu yenu. Lishikilieni. Na sote pamoja tunashikilia jambo moja, nalo ni Mungu.

59 Mshiriki akikosa, msimfukuze; msaidieni, mwinueni, kusanyikeni pamoja, ongeeni ninyi kwa ninyi. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. Tufanyapo kosa, hebu twendeni mbele za Mungu. Kabla hatujaenda mbele za Mungu, yatupasa twende mbele za yule mtu tuliyemuudhi.

60 Ilinibidi tu kutenda hilo. Nami najua kuwa nilikosa, nilidanganya, nilimfanya mke wangu adanganye. Naamini niliwaambieni hayo hapa kanisani. Ilikuwa hivi majuzi si siku nyingi zilizopita, imekuwa kama majuma sita yaliyopita. Wale mawakili walikuwa wamenirarua—rarua kwa ule uchunguzi hadi ilikuwa vigumu kwangu kujua nilikuwa wapi. Nilikuwa tu nishaenda nyumbani toka afisini kula chakula cha adhuhuri, na nambari ya simu yangu ikalia naye Meda akaenda kuijibu. Yeye akaifunika kwa mkono wake, kasema, "Ni wale mawakili tena."

61 Nilisema, "Singevumilia jioni nyingine. Kichwa changu karibu kurukwa na akili. Narukwa na akili, wakinivuta huku na kule na huku," Nilisema, "Siwezi kuvumilia." Nami nikaruka juu, na kusema, "Waambie mimi siko hapa," nami nikakimbia nyuma ya nyumba.

62 Niliporudi, (Meda akiwa anawaza kuhusu mambo hayo), akanikabili mlangoni, nusu akilia, akasema, "Bill, je, hilo lilikuwa jambo zuri kutenda?"

63 Wajua jinsi ulivyo. Najua jinsi nilivyo. Nilisema, "Hakika, sikuwa hapa wakati huo." Nilijua Mungu alikuwa amenihukumu kwa ajili yake. Nikasema, "Sikuwa hapa wakati huo."

Kasema, "Lakini ulikuwa ndani hapa yeye alipopiga simu."

64 Jioni hiyo nilikwenda kumwombea mtoto mgonjwa. Na kabla sijaondoka nyumbani, simu ililia tena na kijana Joseph akaenda akashika simu na kusema, "Baba, wataka niwaambie wewe hauko hapa?" Mwaona jinsi dhambi inavyopotosha, je, ingekuwa jamaa ya aina gani mwishowe?

65 1 Yohana, sura ya 5 na kifungu cha 21, ilisema, "Mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu." Lakini mioyo yetu ikituhukumu, twawezaje kuwa na ujasiri kwa Mungu? Twajua mradi tu tungali na dhambi ambayo haijaungamwa, Yeye hatatusikia. Hilo ni gumu, lakini, ni—ni—ni, kanisa lahitaji mambo hayo.

66 Ndipo nilianza kuombea mtoto huyu. Na nilipoanza kumwekea mikono, Bwana akanikemea na kusema, "Ulisema uwongo, hustahili kumwombea mtoto huyo."

67 Niliondoka kwa huyo mtu, nikasema, "Bwana, ngoja tu hapa. Nina jambo linipasalo kulisahihisha."

68 Nikampigia wakili simu kisha nikaenda afisini, niliingia, na kusema, "Tazama, bwana, nilisema uwongo. Nilimfanya mke wangu adanganye, yeye alisema sikuwa mle ndani. Nami nilikimbia nje nyuma ya nyumba." Nami naliungama na kumwambia kisa hicho.

69 Yeye aliinuka, akaweka mikono yake mabegani mwangu, akasema, "Ndugu Branham, kila mara nimekuwa na matumaini kwako, lakini ninayo zaidi sasa. Mtu" yeye akasema "anayependa kusahihisha makosa yake!"

70 Nami nilimwambia, nilisema, "Nilianza kumwombea mtoto mchanga na Bwana hangeniruhusu. . .alinihukumu moyoni mwangu, kwa sababu nilijua nilikuwa nimekosea."

71 Kisha siku iliyofuata, mke wangu alisema, "Unakwenda wapi?" Nilisema, "Pangoni mwangu."

72 Nami nilikwenda hadi pangoni mwangu hapo juu ya Charlestown, ambapo nimekuwa nikienda kwa miaka mingi, nami niliingia hapo na nikaomba siku hiyo yote, "Ee Mungu, usiniruhusu nikatende jambo kama hilo tena. Unisamehe, Bwana, maana nianzapo kuweka mikono yangu juu ya watu wagonjwa kuomba, ndipo nahukumiwa." Yapata saa tisa jioni nilitoka nje, na kuna mwamba mkubwa ulio nje hapo, nami nikapanda juu ya mwamba huo na nilikuwa nikitazama juu kuelekea mashariki, hali mikono yangu iko juu, nikimsifu Bwana. Na ilikuwa kimya sana ndani humo, nami nilisema, Bwana, ikiwa tu uta. . .Siku moja ulipitia karibu na Musa, ndipo akasema ilikuwa ni wakati ulipomleta yeye katika pengo za majabali, na ilionekana kama mgongo wa mwanadamu. Nilisema, "Je, unaweza kufanya hivyo tena, Bwana, kusudi nijue nimesamehewa?" Nami nilisema, "Ukinisaidia na ukaingie bongoni mwangu." Nilisema "Bwana, mi—mimi hata sina akili nyingi, maana sina elimu." Nilisema, "Na ni—najaribu kukutumikia Wewe. Wajua moyo wangu, nami sikuku. . . Haikunipasa kutenda hilo. Sikutaka kufanya hilo. Nalikuwa karibu kurukwa na akili, nilikuwa na wasiwasi, nami nilitenda hayo wakati wa kunaswa, Shetani aliponishika." Nilisema, "Iwapo utanisemehe hebu ukaniruhusu nikuone basi, Bwana."

73 Mungu akiwa hakimu wangu, papo hapo kando yangu, mahali padogo vijiti vikaanza kuvuma kama upepo, na ukaja kupitia upande wa pango lile nilimokuwa, na ukapitia mwituni. Lo, ndugu, amani ipitayo ufahamu wote ilipitia juu yangu, nami nikapaza sauti, nikalia machozi, nikapiga makelele. Najua nilisamehewa dhambi zangu. Oneni, nilikuwa nimefarakanisha

ushirika wa Mungu, singeweza kupata ukombozi kwa ajili ya mtoto huyo.

74 Na siku iliyofuata kulikuwako mtu fulani toka Chicago, ambaye ni mtu mkuu, Mkatoliki aliyeongoka tu, vilango vya moyo wake vilikuwa vimefura kama mpira wa ndani uliowekwa pumzi, nao walikuwa wamejaribu kuvikata kwa muda mrefu, walikuwa wavikate, naye hakuwakubalia. Mwishowe yeye akapata mahojiano. Katika mahojiano hayo, sisi huendelea tu nayo hadi tugundue ni kipi kibaya. Mara tu yule mtu alipoingia Roho Mtakatifu alimsimulia maisha yake na kutaja jambo fulani yeye alikuwa ametenda alipokuwa toto misa katika kanisa Katoliki. Yeye akasema, "Hayo ni kweli. Hayo ni kweli kabisa." Kasema, "Je, unataka kusema hilo lilikuwa dhidi yangu?"

Nilisema, "Hicho tu ndicho kivuli niwezacho kuona maishani mwako."

75 Akarudi huko na kumwambia daktari, kasema, "Vema, kusanya vyombo pamoja sasa, tutakufanyia na upasuaji."

76 Yule daktari kasema, "Tutauchunguza maskini moyo huo tena." Na alipouchunguza, yeye alisema, "Hauhitaji upasuaji."

77 Mnaona, "Mioyo yetu ikituhukumu." Twahitaji ukombozi mkamilifu. Hatutaki tuwe kanisa nusu. Twataka kuwa Kanisa halisi, au tusiwe kanisa lo lote. Twataka tuwe Wakristo halisi au sio Wakristo kwa vyo vyote vile. Twahitaji ukombozi mkamilifu toka kwa tabia zetu, toka kwa dhambi zetu, toka kwa kuwaza kwetu kuovu, toka kwa matendo yetu maovu, toka kwa kutokujali kwetu, cho chote tulichotenda. Twataka ukombozi mkamilifu, ili watu wajapo kanisani humu kuombewa, kutakuwa tu na kundi hili ndogo (labda si zaidi ya mia moja au mbili) wakiketi hapa lakini wao watakuwa kabisa mikononi mwa Mungu. Na tuombapo, ndipo Mungu atasikia toka Mbinguni. Mungu anataka mtu ambaye Yeye aweza kumshika mkononi mwake, mtu ambaye Yeye aweza kusema, "Nina matumaini kwake. Naweza kumtuma huyu, mtumishi Wangu mgonjwa, kwenye maskani ya Branham huko Jeffersonville, na hilo kundi la watu walio na nia moja." Kitu fulani kitatendeka.

78 Vema, tazameni kile Yeye anachotutendea sisi katika hali tuliyomo, Yeye angetutendeaje kama tungalikuwa na moyo mmoja na nia moja? Na njia pekee tuwezayo kufanya hilo, ni kuunganisha mioyo yetu pamoja katika upendano wa ndugu, kuwatii wahudumu wa kanisa pamoja na mchungaji; naye mchungaji amtii Mungu; ndipo Mungu atafanya kazi kupitia kwa mchungaji, kupitia kwa halmashauri, hadi kanisani, na wote pamoja katika umoja mmoja, kwa ufalme wa Mungu. Naam, Mungu atasikia tutakapokuwa na kundi lililounganika. Usiruhusu cho chote kikuudhi. Usifadhaike katika jambo lo lote.

79 Sasa, hiyo ndiyo aina ya mtu ambaye Mungu alimchagua kuitwaa ile nchi. Musa alikuwa mkamilifu, alikuwa mtu ambaye hangepatana. Ikiwa kulikuwa na mashaka na ugomvi, na kadhalika, yeye hangepatana. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka tuwe sasa.

80 Farao alitaka kukubali, kasema, "Musa, ninyi nyote mwaweza kwenda, lakini acheni wana wenu nyuma, au mkaache baadhi ya ng'ombe zenu humu."

81 Hivyo ndivyo Shetani anavyotaka Wakristo waje. "Itakuwa vema kwako kujiunga na kanisa, bali usimsamehe Yones. Itakuwa vema ikiwa waweza kuingiza yako. . .ikiwa waweza kwenda. . .Haikubidi kuacha uvutaji sigara wako, unywaji pombe wako, kudanganya kwako, kuiba kwako. Masuto yako, kusengenya, haikubidi kuyaacha hayo. Hebu tu jiunge na kanisa."

82 Lakini Musa hakuwa mtu wa mapatano, yeye alitaka ukombozi mkamilifu. Yeye alisema, "Hatutaacha hata ukwato mmoja nyuma. Tutachukua kila kitu kilicho chetu, tuendapo kumwabudu Bwana."

83 Hivyo ndivyo kanisa lipaswavyo kuwa. "Tutachukua haki, tutachukua utakatifu, tutamchukua Roho Mtakatifu, tutachukua kundi lililounganika pamoja, tuendapo madhabahuni. Tutakuwa kundi halisi, hatutaacha cho chote nyuma. Tutachukua kila kitu. Hamna ukwato hata mmoja utakaobaki hapa." Ninyi mwajua, na watu wanaweza kuomba kwa hali kama hiyo hata Shetani ashindwe.

84 Hivyo ndivo Musa na kundi lake walivyofanya. Wao walifika huko na kuingia chini ya damu. Mliona, hadi walipoingia chini ya damu ile hapakuwa na ukombozi mkamilifu. Musa mwenyewe, yeye alikuwa ameunganika pamoja na Mungu. Lakini Israeli hawakuwa vile, wao walikuwa wangali wana dhambi, nao walimnug'unikia Musa, nao walisema, "Naam, mbona unatenda hili? Unatuletea taabu nyingi," kwa sababu Farao alizidisha tu hesabu ya matofali yao na kadhalika. Huyo alikuwa Musa; yeye alikuwa kabisa mikononi mwa Mungu, amekombolewa kabisa toka kwa uchungaji wa kondoo, achunge kondoo wa Mungu; Yeye mwenyewe aliisha kombolewa kabisa; lakini watu hao hawakuwa wamekombolewa, kwa sababu kulikuwa kungaliko manung'uniko kati yao.

85 Usiku mmoja Mungu alipoagiza kuwa mwana kondoo lazima achinjwe, mfano wa Kristo, na ile damu ilichovwa katika hisopo, ambayo ni kwekwe (ya kawaida, nyenyekevu,) na kuwekwa kizingitini mwa mlango, na kwenye miimo, na hapo ndipo Israeli walikombolewa kabisa, bila ukwato ulioachwa nyuma. Mali yao yote ilikombolewa. Jamaa zao, wapendwa wao, na kadhalika vilikombolewa wao walipokuja kabisa chini ya damu.

86 Na hapo ndipo kanisa litakapokombolewa kabisa kikamilifu, kila kitu kitakapokuja chini ya hiyo Damu. Dhambi zako zijapo chini ya Damu, uvutaji sigara wako, uchezaji karata wako, kudanganya kwako, wizi wako, uongo wako, na kila kitu kitakapokuwa chini ya Damu, ndipo kutakuwa na ukombozi mkamilifu. Ikiwa umekosea mtu fulani, rekebisha. Huwezi kuleta hilo chini ya Damu, haliwezi kudumu. Huwezi kulileta. Kitu fulani hakitakuruhusu ulifanye. Wewe mwenyewe utakapokuwa mkamilifu, umeshaletwa kabisa chini ya hiyo Damu, kutakuwa na ukombozi mkamilifu. Ndipo utakuwa na uhuru usiowahi kuujua mbeleni, kila kitu kitakapoletwa chini ya Damu, kuingizwa kwa unyenyekevu katika Ufalme wa Mungu. Ndipo kutakuwa na ukombozi mkamilifu.

87 Yesu alikuwa binadamu kweli kweli na mkamilifu. Yeye angelia kama binadamu, angekula kama binadamu, angekuwa kama binadamu. Alikuwa binadamu halisi kwa vyo vyote vile katika mwili Wake wa maumbile. Na katika Roho Yake, yeye alikuwa Mungu kabisa kwa hivyo aliufanya mwili Wake kumtii huyo Roho aliyekuwa ndani Yake. Mwaona, Yeye alijaribiwa katika hali zote kama sisi. Alikuwa mwanadamu, sio Malaika. Alikuwa mwanadamu! Alikuwa na tamaa na majaribi kama tu sisi tulivyo nayo. Biblia ilisema Yeye alikuwa hivyo. Alikuwa mwanadamu, si Malaika asiyejaribiwa. Waebrania 1 ilisema kuwa Yeye alikuwa hivyo, waebrania 1:4, ilisema Yeye alifanywa Mdogo punde kuliko malaika. Alikuwa mwanadamu mwanadamu kabisa, hivi kwamba Mungu alichukua mwanadamu kabisa kuleta ukombozi mkamilifu; Naye akamjaza Roho Wake, Roho Matakatifu alikuwa ndani Yake pasipo kipimo. Naye alijaribiwa kama sisi. Naye alikuwa Mungu kabisa. Alithibitisha hilo alipowafufua wafu, alipokomesha maumbile, ile bahari iliyokuwa ikinguruma na hiyo tufani kuu. Alipoizungumzia miti, na kadhalika, vilimtii. Yeye alikuwa Mungu, ndani. Naye angalikuwa mwanadamu, kwa kuwa alikuwa mtu, lakini alijitolea Mwenyewe kabisa, (kama mwanadamu) mikononi mwa Mungu, kwa utumishi wa Mungu.

88 Na yeye ni mfano kwetu. Sisi ni wanaume na wanawake. Sisi ni Wakristo pia. Ikiwa Yeye yu mfano wetu, nasi tujikabidhi wenyewe kabisa mikononi mwa Roho Mtakatifu, ili tuwe raia wa Ufalme wa Mungu.

89 Yeye alikuwa mwanadamu kabisa, alikuwa Mungu kabisa, lakini alijitolea zile sehemu Zake za maumbile kwa...na sehemu Zake za mwili, na kuwaza Kwake, na kutenda Kwake, na kujisumbua Kwake, na "Natenda tu kile kimpendezacho Baba." Naam. Kukombolewa kabisa kutoka kwa binadamu. Makuhani walimjia, watu wakuu, na kusema, "Rabi *Fulani wa fulani*," na kujaribu kumpa Yeye rushwa aingie katika makundi yao

na madhehebu, lakini Yeye alifanywa huru kabisa kwa sababu alimtumainia Mungu.

90 Je, si mtunga Zaburi alisema, "Utamwokoa maana Yeye amenitumainia mimi kabisa"? Mwaona? "Nitamwokoa mpenzi wangu toka kwa mbwa, maana Yeye amenitumainia Mimi."

91 Wakati fulani tutakapofika mwisho wa safari ya maisha, nautaka kwa yangu, najua unautaka kwa yako. Namtaka Yeye asema, "Nitamwokoa Yeye toka kwa taya za mauti, maana Yeye alinitumainia Mimi. Nitamwokoa Yeye toka kaburini, asubuhi hiyo ya ufufuo, nitamkomboa kabisa, nafsi, mwili na Roho, kwa sababu Yeye amenitumainia Mimi."

92 Kazi zote za Yesu zilikuwa kamili, kila kitu kilikamilishwa, kilikombolewa kabisa. Yeye alimkomboa kikamilifu yule mwenye ukoma toka kwa huo ukoma. Yeye alimkomboa kabisa mwanamke aliyekuwa na mtoko wa damu kutoka kwa mtoko wake wa damu. Yeye aliukomboa kikamilifu ulimwengu kutoka kwa dhambi, alipokufa ile siku ya upatanisho. Yeye alitakasa kabisa kila dhambi. Alililikomboa kanisa. Kwa hivyo hakuna haja kwetu kuishi kama watu wasio na haki. Hakuna haja kwetu kuishi katika hali ya kushindwa, maana Yeye alimshinda ibilisi na kuchukua mamlaka yote na nguvu na kuviweka chini ya miguu Yake, na havina haki halali kuwatawala nyinyi. Sisi tu Wakristo, tuliojazwa na Roho Mtakatifu. Haitupasi kuamriwa na shetani. Kristo alitukomboa, ukombozi mkamilifu; alitukomboa na maovu, alitukomboa na dhambi, alitukomboa tokana na tabia mbaya, alitukomboa na kusengenyana, alitukomboa toka—toka kwa matusi, alitukomboa toka kwa namna zote za mambo machafu. Yeye alitukomboa kabisa na kutuweka katika mikono Yake mitakatifu, ukombozi mkamilifu kabisa.

93 Yeye alikomboa magonjwa yetu. Alitukomboa toka kwa magonjwa, maana tuna haki Yake ya umilikaji. Haleluya! "Maana Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Yeye yu mponyaji wetu. Hiyo ndiyo sababu maskini mwanamke yule aliyepooza aliyekuwa akijaribu kumtunza mumewe aliyekuwa akifa kwa ugonjwa wa kansa, yeye aliingia katika milki za uwepo wa Mungu. Yeye alikuwa na imani, naye. . .Madaktari walikuwa wamemfanyia yote waliyoweza kutenda, kwa hivyo yeye alifuata maagizo ya Mungu na akakombolewa kabisa.

94 Wanafunzi walikuwa na ukombozi mkamilifu, ukombozi mkamilifu kabisa. Kwa nini? Kwa sababu wao walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu kabisa na kwa ukamilifu. Unapokuwa tu mshiriki wa kanisa na kusalimiana kwa mkono na mchungaji au mengineyo. . .na ulikuwa na baadhi ya ujuzi mdogo wa kurukaruka, ukipiga kelele, au kunena kwa lugha, au kitu kama hicho; na ungali na kijicho moyoni mwako,

matendo yasiyofaa, kusema uwongo, kuvuta sigara, kutamani wanawake, kuna kitu fulani ambacho bado hakijatendeka, kuna kitu fulani kibaya, "maana yeye aupendaye ulimwengu, wala mambo ya ulimwengu, upendo wa Mungu haumo ndani yake." Umepotoshwa. "Kwa matunda yao mtawajua."

95 Sote twataka kuunganishwa pamoja na Roho Mtakatifu. Kila mshiriki yampasa aunganike mmoja na mwingine. Pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu, latuosha toka kwa uovu wote, tumekombolewa toka kwa vitu vya ulimwengu. Yesu alisema, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Ambapo mshiriki mmoja ampenda mshiriki mwingine sana hata angalimfia.

96 Jambo ovu moja lianzapo, ulimwengu wa nje, wanawake fulani huja, kasema, "Sasa, tazama, mpenzi, ni heri utende hiki au tenda kile, vaa hiki au fanya kile, au fanya hiki na ondoka kwa kundi hilo la watakatifu wafingirikao, au mengineyo."

97 Tumeunganika sana na Mungu! Mwasema, "Vema, Ndugu Branham, ni jaribu la kuogofya." Lakini Kristo alikufa kwa kusudi hilo. Shetani ameshindwa. Twataka ukombozi mkamilifu. Twataka kanisa lililo safi na leupe na lisilotiwa najisi, na lililosafishwa katika Damu ya yule Mwana—Kondoo, na limejazwa Roho Mtakatifu, na ishara na maajabu na miujiza. [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kila mtu amekombolewa kabisa. [Nafasi tupu kwenye kanda].

98 Mungu mpendwa, huchukui vitu ila viwe vimekombolewa kabisa. Huwezi kupokea dhabihu iliyo na waa. Hungepokea ombi ambalo kuna dhambi kule nyuma maishani mwa mtu huyo. Hungeweza kufanya hivyo, Bwana. Hukutenda hayo katika nyakati zilizopita, na huwezi kuyatenda sasa. Lakini dhabihu lazima iwe bila waa. Na, Bwana Mungu, tunapojilaza wenyewe madhabahuni kama maisha yaliyotolewa sadaka, chukua toka kwetu, Ee Bwana, mawaa yote ya dhambi. Nitaiweka kabisa nafsi yangu na mwili wangu na nguvu zangu na juhudi zangu, pamoja na kanisa hili asubuhi hii, madhabahuni. Tusafishe kwa Damu Yako, na utusemehe kila dhambi ambayo tumefanya. Na Roho Mtakatifu aliye mkuu na adumu ndani yetu kwa wingi, na Uwepo Wake uende pamoja nasi toka hapa maskanini asubuhi hii, ili tujue ndani yetu kuwa Yeye ametusamehe. Ndipo maombi yatakuwa, "Utusamehe makosa yetu kama sisi nasi tuwasamehavyo waliotukosea." Tujalie, Bwana.

99 Nawe uwe karibu nasi sasa, tubariki na uwe nasi hadi tukutane tena kwa ibada ya jioni. Na tuje tuingie tukiwa na mikono misafi na mioyo mieupe, ambayo hautaikataa maana twataka ukombozi mkamilifu kabisa toka kwa kila kitu, Bwana, ambacho chaweza kutuzuia tusiwe nuru ya ulimwengu; taa iliyo mlimani, si iliyofunikwa na pishi, lakini taa iliyowekwa

mlimani, itoayo nuru ya kuongoza miguu ya watu katika njia inayofaa. Tujalie, Baba. Twaomba katika jina la Yesu, na kwa utukufu Wake. Amina.

100 Nitamuuliza Doc, nadhani yeye yuko nyuma hapo, au mmoja wa mashemasi aliyeko, ili kanisa lipate kusoma haya. Doc, njoo uweke haya kwenye ubao wa matangazo ili kanisa waweze kuyasoma wanapotoka nje. Na ndipo Ndugu Collins, ikiwa yeye yuko hapa . . . Je, Ndugu Collins yuko humu? Mpe hii nyingine.

101 Vema, bwana, nasi tutaona kile . . . [Ndugu Branham atulia kidogo—Mh.]. Huyo ni mtu fulani anayetaka mahojiano. Hilo kila mara hukubaliwa. Tuna furaha. Nami nina mahojiano. Mwaona, jambo la kufanya ni kutupigia simu kule. Tu—tulikuwa na shida nyingi huko nyumbani; vema, kanisa lajua hilo, (huyu ni mgeni,) kanisa linajua hayo yapasa kipande kidogo kiwekwe . . . Nitakiweka hapa kanisani pia, kwa ajili ya wageni. Mwaona, kunao wengi sana, hata tusiweze kuwashughulikia wote, maana wao huja kwa zamu. Mwaona? Nasi . . . Na ikiwa utapiga simu BUtler 2-1519 BUtler. Na washiriki wo wote walio na mtu ye yote atakaye . . . Mimi kila mara hufurahia kuonana na watu, lakini tuna taratibu inayofuatwa. Kunao wengine ambao tayari wamepiga simu, wengi, mnaona, nasi huja mmoja kwa mmoja tunapokuja. Kisha kuna . . . Hapo mbeleni tulikuwa na mpango ovyo ovyo, watu wakija kwa njia yo yote, tukiruka, kutoka, na watu walikwenda nyumbani huku wameudhika na kadhalika. Sasa, kuna utaratibu kwa kila jambo. Na hicho ndicho tunachojaribu kunena juu yake sasa, mwaona, kuweka kila kitu katika utaratibu kabisa. Nami nitafurahi kuona hili kundi ninalopenda, ikiwa watapiga simu BUtler 2-1519, -1519, na Bw. Mercier ama Bw. Goad, mmojawao, ataijibu ile simu na kuwaambia ninyi hasa ni wakati upi mwaweza kupata nafasi. Tuna mahali nje hapo, hewa hurekebishwa ikiwa joto au baridi, na tayari kupokea watu na kuwaombea. Tuna furaha tu kufanya hivyo.

102 Sasa, sababu siji kanisani, watu hudhani mimi huwatoroka watu, sivyo. Najaribu ku—kuwa hasa na utaratibu. Mwaona, hiyo ndiyo sababu nataka kuwa, ili nisionyeshe upendeleo. Kila mtu, mtu ye yote, mahali po pote wakati wo wote, waona; rangi, kanuni ya imani haijalishi. Twaja papa hapa na kukutana na watu. Na, ikiwa wana haja, tunangojea mbele za Mungu hadi Mungu aitosheleze. Na ikiwa wanataka kujua lo lote kuhusu mikutano, naam, sisi hushughulikia hiyo na kuiweka kwenye faili, hayo ni kwa uongozi tu wa Roho Mtakatifu. Na hiyo ndiyo, nafikiri, njia ya haki, kumtendea kila mmoja sawasawa tu na mwingine. Kwa hivyo, hakuna upendeleo, hakuna upendeleo.

103 Kuna watu wo wote waliokuja kuombewa asubuhi hii, waliokuwa wagonjwa na walitaka waombewe? Vema, hakuna? Basi na tuimbe wimbo mzuri kwa—kwa kuabudu. Tutaimba gani asubuhi hii? *"Sioshwi Dhambi Zangu?"* Waujua, Teddy? *"Bila*

Damu Yake Yesu.” Sioshwi. . . [Dada katika mkutano aeleza kuhusu mwanamke aliye “mgonjwa sana.”—Mh.] Vema, dada. Je, wataka tumwombee sasa? Nitamwombea mwanamke huyo. Mwekee mwanamke huyu *hapa* mikono. Mwaweza, tafadhalini, kuinamisha vichwa vyenu pamoja nami kwa dakika moja hivi, kwa utulivu sasa.

104 Mungu mpendwa, kunaye mwanamke aliye mgonjwa sana. Dada yetu ameinua mwili wake juu. . .?. . .hata kuchukua ugonjwa wa kansa toka kwa wengine, amesimama pengoni kwa ajili ya wengine. Lakini wewe wamkomboa toka hayo, Bwana, siku chache zilizopita wakati mambo haya yalipojulikana, na umruhusu ajitambulie mwenyewe basi, Bwana, atajua kuwa yatoka Kwako. Naweka mikono yangu juu yake na kumwombea rehema huyo mwanamke mwingine. Na neema ya Mungu, nguvu za Roho Mtakatifu. . .?. . .mioyo yetu, Bwana. Tufunulie kwanza. . .?. . .Ndipo tunajua kuwa tumependwa na Mungu, tuna amani na Mungu, tunapata kile tunachoomba; kwa sababu hatuna hukumu. Tujalie, Bwana. Katika jina la Yesu naomba, Amina. Asante, mama. Vema.

Sioshwi dhambi zangu,
Bila damu yake Yesu;
Hapendezewi Mungu,
Bila damu yake Yesu.

Hakuna kabisa
Dawa ya makosa
Ya kututakasa
Ila Damu yake Yesu.

105 Ni wangapi wanajisikia kuwa dhambi zenu zote ziko chini ya Damu? Hebu tuuimbe hali mikono yetu imeinuliwa sasa.

Sioshwi dhambi zangu,
Bila damu yake Yesu;
Hapendezewi Mungu,
Bila damu yake Yesu.

106 Sasa tunaposhusha mikono yetu, na tusalimianeni kwa mikono pande zote.

Hakuna kabisa
Dawa ya makosa
Ya kututakasa
Ila Damu yake Yesu.

Mwampenda?

Yesu nakupenda,
Yesu nakupenda,
(Dumuni naye, kila mmoja, jishikilieni kwa
Mungu) Yesu na kupenda,
Kwani ulinipenda.

Sitamwacha kamwe.

Ukombozi Mkamilifu SWA59-0712
(A Total Deliverance)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi Julai 12, 1959, kwenye Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Amerika, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org